

## UCHAMBUZI WA HAKIRASILIMALI KUHUSU BAJETI YA WIZARA YA MADINI NA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19 NA 2019/2020

### 1. UTANGULIZI

Sekta ya uziduaji (Mafuta, Madini na gesi asilia) ni eneo muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya nchi kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuwa sekta ya uziduaji nchini inakadiriwa kuchangia takribani asilimia 5<sup>1</sup> (2018) ya pato la Taifa ambapo, Dira ya Taifa ya maendeleo inakadiria kwamba hadi kufikia Mwaka 2025 mchango wa sekta ya madini unatarajiwa kuongezeka hadi kufikia asilimia 10 ya pato zima la Taifa.



Kwa kuzingatia umuhimu wa Sekta ya uziduaji nchini, HakiRasilimali (Mtandao wa Asasi za Kiraia unaofanya kazi za uchambuzi wa Sera na Uchechemuzi katika sekta ya Uziduaji), umekuwa ukifuatilia kwa karibu na kwa umakini Mwelekeo wa Kisera, mipango, matamko na bajeti ya Wizara husika, na hatimaye kufanya uchambuzi katika maeneo tajwa, hasa kwa kulinganisha hatua mbalimbali za utekelezaji wa sheria, sera, mipango na bajeti husika kwa mwaka uliopita na mwaka uliopo na hatimaye kutoa mapendekezo kuhusu maeneo ya vipaumbele ambayo tunaona yanafaa kuwa sehemu ya mipango na utekelezaji wa bajeti ikjkwa mwaka wa fedha unaofuatia.


Kwa minajili hiyo, kama ilivyo kwa miaka iliyopita, mwaka huu pia HakiRasilimali imefanya mapitio ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka uliopita na hatimaye kujadili na kuchambua kwa kina mwelekeo wa kisera na maeneo mengine pendekezwa kwa lengo la kutoa maoni yetu na pia kuainisha maeneo ya kipaumbele katika bajeti za Wizara ya Madini na Wizara ya Nishati kwa mwaka 2019/2020. Lengo kuu la maoni haya ni kuboresha usimamizi na utekelezaji wa sera,

<sup>1</sup> <https://eiti.org/tanzania>

mipango na mikakati mbalimbali ya Wizara ya Madini na Nishati ili kuleta matokeo yenye tija na endelevu kwa manufaa ya Taifa letu.

## 2. MAPITIO YA BAJETI YA TAIFA 2018/2019 na 2019/20 KWA UJUMLA;

Katika kipindi cha Mwaka 2018/19 Serikali ilipanga kutumia bajeti ya jumla ya Shilingi bilioni **32,476.0<sup>2</sup>** ambapo, Shilingi bilioni **20,468** ilitengwa Kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (recurrent expenditures) na Shilingi bilioni **12,007** ikitengwa kwa ajili ya bajeti ya Maendeleo (Development expenditures).



hizo, Shilingi bilioni 23,045.3 zinatarajiwa kukusanya kutoka katika mapato ya ndani, na tofauti yake itakusanya kutoka vyanzo mbalimbali vikiwemo mikopo na misaada kutoka ndani na nje ya nchi. Halikadhalika, Serikali inakadiria kutumia Shilingi bilioni **20,856.8** kwa Matumizi ya Kawaida, na Shilingi bilioni **12,248.6** kwa ajili ya Matumizi Maendeleo, ambapo, katika bajeti ya maendeleo Shilingi bilioni 9,737.7 zitakuwa ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 2,510.9 zitatoka nje ya nchi.

Kwa kipindi cha kuanzia Julai 2018 hadi Januari 2019, jumla ya Shilingi bilioni 11,006.5 zilikusanya ikiwa ni pamoja na mapato ya kodi na maduhuli mbalimbali, hii ikiwa ni sawa na asilimia 52.7 ya shilingi bilioni **20,890** zilizopangwa kukusanya kwa mapato ya ndani. Katika kipindi hicho pia, jumla ya shilingi **13,750.6** ziliidhinishwa kutolewa na Serikali ambapo, Shilingi bilioni **10,962.1** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni **2,788.5** kwa ajili ya maendeleo. Kwa minajili hiyo, hadi kufikia januari, 2019, ambayo ni robo tatu (3/4) ya mwaka wa utekelezaji, ni asilimia 23.2 tu ya bajeti nzima ya maendeleo ilikuwa imetolewa kwa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo nchini.


## MWAKA 2019/2020:

Katika Makadirio ya bajeti ya mwaka **2019/2020**, Serikali imepanga kukusanya na kutumia Shilingi bilioni **33,105.4<sup>3</sup>** kati ya

<sup>2</sup> **Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

<sup>3</sup> Chanzo: Wizara ya Fedha

Kwa ujumla, makadirio ya bajeti ya Mwaka wa fedha 2019/20 ina tofauti ya ongezeko la takribani Shilingi bilioni 629.4 ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka 2018/2019. Kwa upande wa bajeti ya maendeleo, Serikali inakadiria kutumia shilingi bilioni **12,248.6** ilinganishwa na Shilingi bilioni **12,007.0** kwa Mwaka wa fedha uliopita, hii ikiwa ni ongezeko la shilingi **Milioni 241.6**.



#### **CHANGAMOTO KATIKA BAJETI YA TAIFA KWA UJUMLA:**

Mwenendo wa utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha uliopita na miaka mingine iliyopita, fedha ya bajeti ya maendeleo imekuwa ikitolewa kidogo ukilinganisha na bajeti ya matumizi ya kawaida. Kwa mfano, hadi kufikia Januari 2019, robo ya tatu ya utekelezaji wa mwaka wa fedha husika, ni shilingi bilioni **2,788.5** tu zilitolewa katika shughuli za miradi sawa na asilimia 23.2 ya bilioni 12,007 iliyoidhinishwa na bunge. Ufinyu wa bajeti ya maendeleo ni kikwazo kwa miradi mingi yenye maslahi kwa wananchi ambayo iwapo rasilimali fedha hazitatolewa inaweza isitekelezeke kabisa au isitekelezwe kwa wakati.


Tunaitaka na kuishauri Serikali, kuipa kipaumbele bajeti ya maendeleo sambamba na kutoa fedha zinazohitajika kwa wakati. Vivyo hivyo, tunasisitiza Serikali kuendelea kutengeneza mazingira ya kuvutia ya kibiashara na kutanua wigo wa kodi na vyanzo mbalimbali vya mapato ili kukidhi mahitaji ya kibajeti.

#### **MAKADIRIO NA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MADINI KWA MWAKA 2018/2019 NA 2019/2020**

Makadirio ya bajeti iliyopitishwa na Bunge kwa ajili ya Wizara ya Madini kwa Mwaka 2018/2019 yalikuwa ni jumla ya Shilingi **58.9 Bilioni**<sup>4</sup>, ambapo **Shilingi 39.2 Bilioni** sawa na asilimia 66.7


<sup>4</sup> Chanzo: Wizara ya Madini

ilikuwa ni kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 19.6 Bilioni** sawa na asilimia 33.3 ikiwa ni kwa ajili ya Matumizi ya maendeleo.




Hadi kufikia Februari, 2019, kiasi cha shilingi **23.4 Bilioni** kilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya kawaida na Matumizi mengineyo, ikiwa ni sawa na asilimia 59 ya lengo la bajeti nzima ya Matumizi ya kawaida (39,287,517,992) ikilinganishwa na Shilingi 100,000,000 zilizopokelewa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ambayo ni sawa na asilimia 0.5 ya lengo la bajeti nzima ya maendeleo. Hata hivyo, Wizara ya Madini ilipokea ruzuku ya shilingi 1, 000, 0000,000 kwa ajili ya ujezi wa ofisi za madini ambazo hazikuwepo katika bajeti ya mwaka husika. Ufinyu wa bajeti kwa ajili ya maendeleo unakwamisha mipango mingi ya maendeleo ya wizara kwa mwaka kutokutekelezeka au ikatekelezeka kwa kiwango cha chini kama ilivyotarajiwa. Hii haitakuwa na tija kwa miradi ambayo inagusa uwezeshejaji wananchi hasa wachimbaji wadogo wadogo.

## Tathmini ya makusanyo ya maduhuri Wizara ya Madini mwaka 2018/19 Na 2019/20



NB:

Taarifa ya Mkaguzi na Mdhitbiti wa Hesabu za Serikali inayoishia Juni 2018, iliyotolewa rasmi Machi 2019, inaonesha kuwa, hadi kufikia June 30, 2018, kulikuwa na baki ya **Dola za Marekani 622,175 na Shilingi 130,331,274.45** katika Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) zilizobaki kutoka sehemu ya ruzuku ya **Dola za Marekani 3,000,000**, ambazo zilitolewa na Benki ya Dunia kwa Wizara ya Nishati na Madini (2015/16) kwa ajili ya kuendeleza Rasilimali madini nchini ili zitolewe kama ruzuku kwa wachimbaji wadogo wa madini ili kuenedeleza uchimbaji mdogo. Hata hivyo, hakkuwa na maelezo yoyote kutoka Wizarani kuhusu fedha hizo ambazo zingeweza kuwa msaada kwa wachimbaji wadogo.



## MAKADIRIO YA BAJETI NA TAASISI ZA WIZARA YA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 NA 2019/2020

### 1. Tume ya Madini

Tume ya Madini imeundwa kwa mujibu wa Sheria ya madini 2010, Sheria ya marekebisho Anuai No. 7 ya Mwaka, 2017. Mamlaka ya kuianzisha Tume na majukumu yake yameainishwa katika kifungu cha 21 na kifungu cha 22, ambapo, mionganoni mwa majukumu ya Tume hiyo ni kusimamia, kuratibu, kupanga, kudhibiti na kutekeleza masuala na shughuli zote zinazohusu madini na pia kuishauri Serikali kuhusiana na shughuli zote zinazohusu Sekta ya Madini nchini. Halikadhalika, Tume ya madini ni chombo chenye mamlaka kamili ya kushitaki au kushitakiwa pale inapobidi.

Katika Mwaka wa fedha wa 2018/19, Tume ya Madini ilikuwa na bajeti ya jumla ya **shilingi 12.5 Bilioni**, ambapo, **shilingi 8.6 Bilioni** ikiwa ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo na **shilingi 3.9 Bilioni** kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Tume. Hadi kufikia Disemba 2018, Tume ilipokea jumla ya shilingi bilioni 8.2 ikiwa ni sawa na asilimia 94 ya lengo la nusu Mwaka wa bajeti husika.

Katika makadirio ya Mwaka wa fedha 2019/20, Tume ya Madini inatarajia kutumia **shilingi 21,404,963,891** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hii inajumuisha **shilingi 13,396,281,500** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **shilingi 8,008,682,391** kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Tume ya Madini<sup>5</sup>.

Changamoto kubwa ambayo inaikabili tume ni kutokuelewaka kwa sheria ya madini kwa wadau wa madini na wafanya biashara ambao husababisha ugumu kwa Tume kukusanya baadhi ya tozo mbalimbali zinazotakiwa kwa mujibu wa sheria ya Madini.<sup>6</sup>

**PENDEKEZO:** Tunashauri Tume ya Madini kuwa na mkakati kabambe wa kutoa elimu kwa Umma mara kwa mara na kutumia njia mbalimbali kama vile televisheni, redio za kitaifa na kijamii pamoja na mitandao ya kijamii n.k. ili Umma watanzania uelimike kuhusu Sheria ya Madini na kazi na mamlaka ya Tume ya Madini.


### 2. Taasisi ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania (TEITI)

Mpango wa Uwazi na Uwajibikaji Tanzania katika sekta ya Mafuta, gasi na madini, umeanzishwa chini ya Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji ya Mwaka 2015 kwa lengo la kukuza na kuboresha Uwazi na uwajibikaji katika uvunaji wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia. Mpango huu unaratibiwa chini ya Wizara ya Madini. Tangu kuianzisha kwake, taasisi hii imekuwa ikikabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo kutokuwa na vyanzo vya uhakika vya fedha katika kutekeleza mipango na shughuli zake mbalimbali.

<sup>5</sup> CHANZO: Vitabu vya Bajeti Wizara ya Madini / Tume ya madini

<sup>6</sup> Chanzo: Taarifa ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya wizara ya Madini kwa Mwaka 2017/18

Katika mapitio ya taarifa ya shughuli zilizotekelawa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019, taasisi hii imeshindwa kutekeleza shughuli nyingi zilizopagwa kutekeleza kwa mwaka husika kutokana na uhaba wa rasilimali fedha. Katika mwaka wa Fedha wa 2018/2019 jumla ya shilingi 1,629,379,543 zilitishwa na Bunge kuitia Wizara Madini, ambapo, matumizi mengineyo yalikuwa ni Shilingi 243,415,543 na matumizi kwa ajili ya maendeleo ilikuwa ni shilingi 1,3385,964,000. Hata hivyo, hadi kufikia februari, 2019, inaonekana hakukua na fedha yoyote iliyotolewa kwa ajili ya maendeleo kwenda TEITI.<sup>7</sup>



Halikadhalika, baadhi ya shughuli zilizotekelawa kupitia TEITI hazina maeleo ya kutosha kuhusu vyanzo vya fedha vilivyofanikisha utekelezaji huo. Kwa ujumla, taarifa ya utekelezaji ya shughuli za taasisi kwa mwaka ulipita haikutoa ufanuzi wa kina kwa baadhi ya masuala ambayo ni muhimu kujulikana na wadau mbalimbali wa maendeleo. Baadhi ya masuala yaliyojiteza katika taarifa ya taasisi ni kama yafuatayo:-

- 1) Taarifa haikuonesha au kufafanua kwa kina kuhusu matumizi mengineyo katika bajeti (OC) yalitumika katika matumizi gani hasa kutokana kwamba taasisi haikupokea kiasi chochote cha fedha kwa ajili ya shughuli za maendeleo.
- 2) Taarifa kuu ya TEITI ya utekelezaji kwa mwaka 2016/17 na 2017/18 hazijatolewa hadi leo, ingawa, kuna maeleo ya kuanza kwa utaratibu wa kumtafuta mtaalamu mshauri wa kuanda taarifa husika. Ingekuwa vyema kwa TEITI kutoa mrejesho wa hatua zilizofanyika katika kutekeleza jukumu la utolewaji wa taarifa jatwa.
- 3) Kuanzishwa kwa rejista ya taarifa kwa Umma kuhusu wamiliki wa hisa katika kampuni za madini, mafuta na gesi asilia ni moja kati ya shughuli iliyopaswa kutekeleza, ila hakuna maeleo yoyote katika taarifa kuhusu hatua za utekelezaji wa uanzishwaji wa rejista hiyo kama ilivyositisizwa na aliyekuwa Waziri wa Madini, Mh. Agella Kairuki tarehe 25/10/2018, jijini Dodoma wakati akizindua kamati ya tatu ya TEITI. Rejista ina umuhimu mkubwa katika

<sup>7</sup> CHANZO: Vitabu ya Bajeti ya Wizara ya Madini / TEITI

kuboresha uwazi katika sekta hii na pia itasaidia kuzuia upotevu wa rasilimali na mapato yatokanayo na rasilimali madini, mafuta na gesi asilia. TEITI haina budi kutoa mrejesho kwa Umma kuhusu hatua iliiyofikiwa ya uanzishwaji wa rejista.

- 4) Taarifa ya TEITI imeonesha mionganoni mwa mafanikio kwa mwaka 2018/19 ilikuwa ni kuongezeka kwa uwazi wa matumizi ya mapato ya halmashauri yanayotokana na tozo kutoka kampuni za uchimbaji madini, mafuta na gesi asilia. Ingawa hakuna maelezo ya kutosha kuonesha ni halmashauri zipo na iwapo ongezeko hilo ni kwa kiasi gani ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita. Ni vizuri kwa TEITI kutoa taarifa zenye maelezo ya kutosha ili kusaidia watumiaji wa taarifa kuelewa kwa kina.



#### Mapendekezo na Ushauri kuhusu TEITI

Kama ilivyoainishwa, mionganoni mwa changamoto kuu zinazo ikabili TEITI ni uhaba wa rasilimali fedha za kutekeleza shughuli za maendeleo iliyojipangia na pia upungufu wa rasilimali watu kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya taasisi. Vivyoohivyo, muundo na mfumo wa

kimamlaka, kiutendaji, kimaamuzi na utashi wa kisisasa vinaweza pia kuwa sehemu ya changamoto za kufikia azma na lengo la kuanzishwa TEITI.

- a) Awali ya yote, tunaipongeza sana Serikali kwa dhamira njema ya kuanzisha na kulea mpango huu kabanbe wenyе tija kwa nchi yetu, tuna imani kubwa na nia ya Serikali na wadau wengine wa maendeleo katika kuifanya TEITI kuwa imara zaidi na yenye kuwajibika ipasavyo. Ni imani yetu kwamba, changamoto zilizojitokeza zimetoa fursa ya kujitathmini na kujipanga vyema kwa ajili ya kufikia malengo tarajiwa. Kwa minajili hiyo, tunapenda kupendekeza yafuatayo;
- b) Serikali ifanye marekebisho ya Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika rasilimali za madini, mafuta na gesi asilia ya Mwaka 2015 ili kuiwezesha TEITI kuwa Taasisi ilio huru na yenye muundo na mfumo mpana unaoiwezesha kuwa na mamlaka katika kukusanya rasilimali fedha na kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati.
- c) Pamoja na kutumia televisheni, na redio, TEITI inapaswa Kutumia njia mbadala katika kuhabarisha na kutaarifu Umma na wadau mbalimbali kuhusu kazi, wajibu na shughuli za TEITI, ingekuwa vyema kuanza kutumia mitandao ya kijamii na redio za kijamii (social media and community redio) ambazo zipo karibu na watu wa rika tofauti na pia hutumiwa na watu wengi zaidi.

- d) Serikali (kupitia Wizara ya madini) iharakishe mchakato wa upatikanaji wa taarifa na Uwazi wa Mikataba ya Madini, gesi na rasilimali zingine kwa kuzingatia kwamba, msingi mkuu wa kuanzishwa TEITI ni kwa ajili ya kukuza na kuboresha Uwazi na uwajibikaji katika uvunaji wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia.
- e) TEITI itoe taarifa kuhusu maendeleo ya uchunguzi wa ukaguzi maalum wa Shilingi bilioni 30.5 kama ilivyojitekeza katika taarifa ya mshauri mwelekezi.
- f) TEITI iharakishe upatikanaji wa watumishi wenyewe uwezo na sifa zinazohitajika katika kutekeleza majukumu ya TEITI katika ngazi tofauti.
- g) Wizara ya madini iwajibike ipasavyo kufanikisha upatikanaji wa rasilimali fedha ili TEITI iweze kuwa na fedha zinazohitajika kutekeleza shughuli za maendeleo kama ilivyopangwa.

### 3. Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

STAMICO ni moja kati ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini. Hili ni shirika linalomilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja, ambalo lilianzishwa rasmi mwaka 1972 chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma (1969). Mwaka 2015 Shirika lilifanyiwa marekebisho makubwa ya kimundo (restructuring) chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma (mabadiliko ya uanzishwaji wa mashirika ya Umma) 2015. STAMICO inamiliki makampuni kadhaa ya madini yakiwemo STAMIGOLD, Buhemba Gold, Makaa ya Mawe Kiwira n.k, kwa lengo la kuyaendesa kifaida.

Katika makadirio ya mwaka wa fedha wa 2018/2019, jumla ya shilingi bilioni 13.6 ziliombwa kupitia Wizara ya Madini kwa ajili ya maendeleo, ambapo, takribani shilingi bililion 9 zikiwa kwa ajili ya maendeleo ya miradi ya Kiwira na Buhemba na shilingi bilioni 4 na zaidi zikiwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hatahivyo, katika kipindi hadi kufikia Februari, 2019, STAMICO ilipokea shilingi bilioni 2.7 tu ambazo zilikuwa ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na matumizi mengineyo. Hii ina maana kuwa, ni asilimia 32.6 tu ya fedha zote zilizopokelewa kwa mwaka wa fedha uliopita.

#### Changamoto zinazoikabili STAMICO



Miongoni mwa changamoto zinazoikabili STAMICO ni (1) uhaba wa rasilimali fedha zinazohitajika kuendesa shirika. Kwa mujibu wa taarifa ya ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG 2019) STAMIGOLD kampuni tanzu ya STAMICO, imekuwa inajиendesa kwa hasara takribani miaka 3 iliyopita kutohana na madeni, uwekezaji mdogo na kampuni kutofanya shughuli za uzalishaji.

(2) Na kwa miezi kadhaa STAMIGOLD Kampuni tanzu ya STAMICO pia imekuwa inafanya shughuli zake kwa inakadiliwa kutumia mafuta ya petrol kisasi cha lita 450 kwa mwezi. Hii ni baada ya kukosa umeme kuendesa shughuli zao.

(3) Vivyo hivyo, Kifungu namba 9 cha marekebisho ya Sheria ya Madini 2010, kupitia Sheria ya marekebisho Anuai sheria No. 7, 2017, Sheria inaelekeza umiliki wa Serikali usiopungua asilimia 16 katika makampuni ya madini, ingawa, sheria au kanuni hazitoi mwongozo kuhusu mamlaka ipi ya Serikali itahusika na jukumu la kusimamia umiliki huo.

### Mapendekezo/ ushauri kuhusu STAMICO

Pamoja na changamoto zinazozikabili Shirika la Madini la Taifa, tunaona mustakabali mzuri wa Shirika katika miaka ijayo, hata sasa, tunatambua jitihada za Wizara na Serikali kwa kulihuisha Shirika hadi kufika hapo lilipo, bado tunaamini kuwa kuna nia ya dhati ya kulifanya Shirika kuwa imara zaidi na kujiendesha kwa faida. Hivyo basi, kwa kutambua umuhimu wa STAMICO katika maendeleo ya rasilimali madini nchini, tunapenda kutoa mapendekezo yetu kama ifatavyo; -


- Serikali ifanye uwekezaji mkubwa kwa STAMICO (pamoja na kuipa ruzuku ya upendeleo) na pia kuchukua dhamana ya madeni yanayoikabili ili iweze kuwa na uwezo wa kujiimarisha kifedha ili kumudu gherama za uzalishaji.
- Tunapendekeza kuwa STAMICO ifanyiwe mabadiliko makubwa ya kimuundo na kimfumo ili iwe kampuni hodhi (Holding company) inayoweza kumiliki hisa au sehemu ya umiliki katika makampuni mengine ya migodi na pia iweze kukuza mtaji kwa kuingia makubaliano ya kimkakati na ya kiuwekezaji, ikiwezekana, kukopa na hata kukaribisha wadau (hasa wananchi) wenye nia ya kuwekeza katika vipaumbele vya Shirika.
- Tunaamini kuwa, iwapo STAMICO itabdalishwa na kuwa kampuni hodhi, itasaidia kukuza mtaji wake kwa haraka, pia itamwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali kufanya ukaguzi (katika mashirika ya Umma na makampuni binafsi (kwenye sekta ya madini, mafuta na gesi asilia) na hatimaye kuweza kujiridhisha na mwenendo wa mapato na matumizi ya makampuni hayo ambayo kwa sasa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali hana uwezo wa kuyakagua kwa mujibu wa sheria.
- Tunapendekeza kuwa, STAMICO ifanyiwe mabadiliko na ipewe jukumu la kusimamia na kuratibu umiliki wa asilimia 16 za Serikali katika makampuni ya madini kwa niaba ya Serikali.
- Tunapendekeza pia, STAMICO ijitanue na kufanya utafiti na uwekezaji katika aina tofauti za madini kama vile "graphite", coal" na mengineyo kuliko kujielekeza zaidi katika dhahabu

### BAJETI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 NA 2019/2020

Katika mwaka wa Fedha wa 2018/2019, Wizara ya Nishati ilikadiria kukusanya na kutumia Shilingi 1.69 Trilioni<sup>8</sup>, katika makadirio hayo, shilingi 1. 665 trilioni zilitengwa kwa ajili ya Maendeleo na Shilingi 27,145,014,000 zikiwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Disemba 2018, kiasi cha shilingi bilioni 275.40 zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya shughuli za maendeleo, hivyo hivyo, Shilingi bilioni 12.1 zikiwa zimepokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida.<sup>9</sup>

<sup>8</sup> Chanzo: Wizara ya Nishati

<sup>9</sup> Taarifa ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini




Katika Mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara imekadiria kutumia **Shilingi 2.142 trillioni** ambapo kati ya makadirio hayo, **Shilingi 2.116 trillioni** ni kwa ajili ya maendelo na shilingi **26.339 bilioni** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida. Vyanzo vya mapato ya bajeti vinatarajiwa kuwa vya ndani na pia kutoka nje ya Nchi, ambapo, Serikali inatarajia kukusanya **shilingi 1,956,372,000,000** kutoka vyanzo vya ndani na pia **Shilingi 160,082,000,000** kutoka nje ya Nchi.



maduhuli kwa mwaka wa Fedha 2018/19.


Kwa mujibu wa takwimu za wizara, makusanyo ya Maduhuli yanayotarajiwa kukusanya kwa mwaka wa Fedha 2019/20 ni billion 612,370,725,000, ikiwa sawa na ongezo la asilimia 55.5 kwa mwaka wa Fedha 2018/19 (Bilioni 394,450.860, 600). Hata hivyo, taarifa ya Wizara haioneshi ni kiasi gani cha Maduhuli kimekusanya kwa mwaka wa Fedha uliopita. Tunaishauri Wizara itoe taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na makusanyo ya

Makadirio ya bajeti kwa mwaka huu wa fedha, yameongezeka kwa takribani asilimia 26 ikiwa ni kutokana na kiasi kikubwa kwenda katika mradi wa rufiji unaotarajia kuzalisha Megawati 2,115, ambapo gharama za mradi zimepanda kutoka **shilingi 700,000,000** kwa Mwaka 2018/2019 hadi **Shilingi 1,443,264,000,000** ambalo ni ongezeko la asilimia **106.2**.



Hivyo basi, tafsiri ya bajeti kwa Mwaka huu inaonesha kwamba, zaidi ya nusu ya bajeti ya Wizara nzima ya Nishati, yaani **asilimia 74** imeelekezwa katika mradi wa Rufiji amba ni mradi kwa ajili ya maendeleo. Tunapenda kuipongeza Wizara kwa kuwa ya mfano kwa kutenga kiasi kikubwa katika bajeti ya maendeleo kwa miaka miwili mfululizo, pia ponezi kwa Serikali kwa nia njema ya kuwekeza katika mradi wenye lengo la kuondoa changamoto za umeme Nchini.

### MGAWANYO WA FEDHA ZA NDANI ZINAZOKUSUDIWA KWENYE MIRADI YA MAENDELEO-WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20



## Mapendekezo:

Pamoja na kutambua jitihada njema za Serikali, Tunashauri kuwa Serikali itoe kipaumbele katika kutenga rasilimali fedha za kutosha katika miradi mingine ambayo ipo katika hatua tofauti tofauti za utekelezaji hasa miradi ya gesi asilia, ili utekelezaji wake uende sambamba na miradi mingine.

### TATHIMINI YA BAADHI YA TAASISI CHINI YA WIZARA YA NISHATI

#### 1. Shirika la Taifa la Maendelo ya Petroli (TPDC)

Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015, inatoa madaraka kwa TPDC kufanya na kusimamia shughuli za utafutaji, uendelejazi na usambazaji wa Mafuta na Gesi Asilia Nchini. Pamoja na umuhimu wa mamlaka ya TPDC bado inakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo zifuatazo;

**Changamoto za Madeni na Ukusanyaji usioridhisha wa wadaiwa:**



#### UENDESHAJI KIASARA:


Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG): Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonesha kuwa hadi kufikia Juni 30, 2018, TPDC ilipata hasara ya Shilingi 64,543,000,000 huku ikiwa na madeni yanayofikia shillingi 3,544,892,000,000 hivyo kuwa katika moja ya mashirika yeye hali mbaya ya kifedha. Halikadhalika, taarifa ya kamati ya Bunge ya Nishati na Madini inaonesha kuwa, hadi kufikia Disemba 2018, TPDC ilikuwa inadai (TANESCO, SONGAS, Ndovu Resource Ltd, Kilimanjaro Oil Ltd n.k) jumla

ya shilingi bilioni 527.096. deni ambalo limesababisha makampuni yenyе mkondo wa juu kutishia kuzuia kuuza Gesi Asilia kwa TPDC kwa sababu ya kushindwa kulipia Ankara zake kwa wakati.

#### UWEKEZAJI KWA AJILI YA SHUGHULI ZA MAENDELEO:

Ufinyu wa bajeti na uwekezaji mdogo TPDC: Hii changamoto ni mionganii mwa sababu zinazokwamisha ufanisi katika utekelezaji wa mikakati inayojiwekea. Mwaka 2016, TPDC iliandaa

Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia (NGUMP 2016 – Natural Gas Utilization Master Plan). Mpango huu ulioainisha kwa kina usambazaji wa Gesi Asilia Nchini. Hata hivyo, mpango huu umekua ukisucasua kutekelezeka hadi leo kwa sababu ya ukosefu wa rasilimali fedha.



ucheleweshwaji wa uwekezaji wa mitaji ya kigeni (FDI) ambayo ni kichocheo cha uchumi na maendeleo ya miradi mbali mbali nchini. Lakini pia upatikanji wa FDIs ungeisaidia Serikali kuelekezarasimali zaidi katika sekta zilizo na ufinyu wa Bajeti hasa katika maeneo ya kimkakati ya kijamii.

### UTEKELEZAJI WA MIRADI YA GEsi ASILIA NA MAKADIRIO YAKE 2018/2019 – 2019/20

- **Mradi wa kusindika Gesi Asilia kwenye hali ya kimiminika (Liquefied Natural Gas – LNG):** Mradi huu umepangwa kutekelezwa kwa Mwaka 2019/20, ambapo bajeti ya **Shilingi bilioni 6.5** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza ulipaji fidia, kufanya tafiti mbalimbali za kiuchumi ili kusaidia timu ya Serikali katika majadiliano na wawekezaji. Mradi huu ulipendekezwa kama ulivyo kwa Mwaka 2018/19 kwa bajeti ya **Shilingi bilioni 6.5**. Mradi huu umekuwa katika majadiliano tangu miaka 2 iliyopita na hakuna taarifa za kutosha kuhusu maafikiano na hatua zilizofikiwa katika majadiliano baina ya Serikali na wawekezaji. Tunaihauri Serikali kuzingatia muda na pia tunaitaka Serikali kutolea ufanuzi wa bajeti inayopangwa kila mwaka na ufanisi wake.
- **Ujenzi wa Miundombinu ya Usambazaji wa Gesi Asilia katika Jiji la Dar es Salaam:** Mradi huu unalenga kujenga miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika jiji la Dar es Salaam. Bajeti ya **Shilingi 1,100,000,000** zimetengwa kwa Mwaka 2019/20. Ingawa mradi kama huu uliwekwa pia katika bajeti ya Mwaka 2018/19 ambapo bajeti ya **Shilingi Bilioni 2** zilitengwa. Hadi sasa hakuna maelezo wala taarifa ambayo imetolewa kuhusu hatua za usambazaji wa gesi asilia katika maeneo husika.

**MAJADILIANO YASIYO NA KIKOMO:** kwa kipindi kirefu sana, kupitia taarifa zinazotolewa na Wizara ya Nishati, kumekuwepo kwa majadiliano yasiyo na kikomo kwa Serikali na Wawekezaji. Hii inaathiri utekelezaji wa mikakati ya baadhi ya shughuli za Gesi Asilia iliyopo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kwa Mfano Utelezaji wa Mradi wa Kusindika Gesi Asilia kwenye Hali ya Kimiminika (Liquefied Natural Gas Plant-LNG).

Vivyo hivyo majadiliano haya yasiyo na kikomo, yanababisha

- **Mradi wa Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Dar es Salaam Tanzania hadi Uganda:** Mradi huu unahusisha ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kwenda Nchini Uganda kutokea Dar es Salaam, bomba hilo litakwenda sambamba na bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki linalotoka Hoima Uganda hadi Chongoleani-Tanga (Tanzania). Bajeti ya **Shilingi 800,000,000** zimetengwa kwa Mwaka 2019/20. Hatahivyo, mradi huu pia ultengewa **Shilingi Bilioni 1.5** katika Mwaka 2018/19 kwa ajili ya Upembuzi Yakinifu. Tunashauri Serikali kufafanua bajeti nzima kwa ajili ya mradi huu na pia kutoa ufanuzi wa hatua za utekelezaji wa bajeti zinazopangwa kila mwaka.
- **Mradi wa bomba la kusafirisha Mafuta ghafi la Africa Mashariki kutoka Uganda hadi Tanga Tanzania (EACOP):** Mradi huu ni mwendelezo wa ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Nchini Uganda hadi Tanzania, ambapo, bajeti ya **Shilingi 7,000,000,000** zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha majadiliano ya kimkataba kati ya Nchi washirika Uganda na Tanzania) na makampuni yaliyowekeza kwenye mradi huu (Total SA na Tullow Plc). Hata hivyo, katika bajeti ya Mwaka 2018/19, **Shilingi bilioni 54** zilitengwa kwa ajili ya kazi na majukumu yanayofanana na mwaka huu. Pamoja na jitihada za Serikali katika mradi huu, ili kukuza Uwazi na Uwajibikaji katika utekelezaji wa mradi huu, tunafahamu majadiliano haya yamechukua sura mpya na hivyo basi tunaishauri Serikali iweke wazi hatua za makubaliano zilizofikiwa hadi sasa, na kipi kinakusudiwa kwenye majadiliano haya mapya. Pia ijulikane jumla ya fidia zitakazolipwa na mchangano wa kila Nchi wabia katika utekelezaji wa Mradi.

## MAMBO YALIYOJITOKEZA KWA UJUMLA

### A. MWELEKEO WA KISERA

HakiRasilimali inatoa pongezi nyingi kwa Serikali na Mamlaka zake kwa hatua mbalimbali ambazo zimechukuliwa katika Utungaji na utekelezaji wa Sheria na Kanuni zinazogusa Sekta ya madini, mafuta na gesi asilia nchini. Katika hatua tofauti, tumeshuhudia Maelekezo kadhaa yakitolewa na Viongozi wa Serikali yenye lengo la kurekebisha kasoro mbalimbali zilizokuwepo pia na kuharakisha utekelezaji wa maudhui yaliyomo katika Sheria ya Madini ya 2010 na Marekebisho yake ya Mwaka 2017.



2017 na vilevile, msukumo zaidi uwekwe katika uvezeshaji wa kifedha na kiufundi na pia usimamizi katika utekelezaji wa Sheria na Kanuni mbalimbali za Madini ili kutekeleza usimamizi madhubuti wa rasilimali madini kwa ajili ya kuwanufaisha wananchi na Nchi kwa ujumla.

Kwa hiyo basi, matarajio yetu kama Asasi ni kuona maamuzi na uelekeo wa kisera katika sekta ya madini, mafuta na gesi asilia unalenga kujenga mifumo imara na taasisi endelevu, inayotoa wigo mpana wa ushiriki wa wananchi kwa ujumla,

#### B. UKAGUZI WA FEDHA NA TAARIFA KWENYE SEKTA YA UZIDUAJI

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, imebaini Changamoto kwa ofisi yake Kupata taarifa za kifedha na kimikataba kutoka katika mashirika na makampuni kwenye sekta ya madini, mafuta na gesi asilia. Changamoto hizi zimesababisha ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali kushindwa kufanya ukaguzi wake kwa mujibu wa Sheria<sup>10</sup>.


Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ana nafasi ndogo sana ya kufanya ukaguzi kwenye makampuni ya uziduaji, kinyume cha Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na kifungu cha 5 na 15 cha Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma yam waka 2008,

Pia tunatambua nakupongeza hatua ya Serikali ya kukutana na wadau na machimbaji wadogo wa Madini nchini kwa lengo la kusikiliza kero, changamoto na maoni yao kuhusu uendelezaji wa Sekta ya Madini. Vivyo hivyo, hatua zilizochukuliwa hadi za kufuta Kodi ya ongezeko la thamani (VAT) 18% na Kodi ya zuio (withholding tax 5%) kwa wachimbaji wadogo, Kufungua na kujenga masoko ya madini katika mikoa yenye uzalishaji wa madini, pia, tamko la Serikali la kurudisha Umiliki wa machimbo ya Makaa ya Mawe Kiwira Serikalini sambamba na kulipa malimbikizo ya Madeni ya TANCOAL Co.

Hatahivyo, tunaona umuhimu wa kuzidi kusisitiza na kushauri Serikali kufanya marekebisho kwa baadhi ya Sheria zinazogusa maendeleo ya Sekta ya Madini (TEITA Act, 2015, 2017 Natural Wealth and Resource; The Permanent Sovereignty Act

<sup>10</sup>The CAG office has a limited scope in auditing the extractive industry companies, contrary to Article 143 of the Constitution of Tanzania and sections 5 and 15 of the Public Audit Act 2008, with respect to accessing information and persons.

juu ya upatikanaji wa taarifa na watu. Vifungu hivi vya sheria vinaingiliwa na kifungu cha 26 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na mabadiliko yake yam waka, na kifungu cha 93 cha Sheria ya Mafuta ya mwaka 2017, vifungu ambavyo vinakataza taarifa a makampuni ya madini na mafuta kutolewa kwa mtu wa tatu isipokuwa tu kwa ridhaa ya wamiliki wa mgodi au wa leseni au haki ya uchimbaji. Ibara ya 18 (k) ya makubaliano ya mfano ya kubadilishana taarifa za utekelezaji (the model production sharing agreement of 2013 (MPSA 2013) yanaruhusu serikali kuitia kwa wawakilishi wake waliopewa nguvu kupata taarifa za mikataba. Ofisi ya CAG iliomba taarifa kutoka Wizara ya Nishati na Kampuni ya Taifa ya Mafuta (TPDC) na kuchukua takribani miezi miwili, mnamo mwisho wa mwezi Februari na kuchangia kushindwa kwa CAG kufanya ukaguzi wa rekodi za kampuni kwenye allowable and receivable costs na mapato yaliyopatikana ili kuweka kwenye ripoti yam waka 2016/17.



Hivyo basi , ili kuweza kuchoea ongezeko la uwazi na uwajibikaji kwenye sekta, kuna haja ya kupitiwa upya kwa sheria ya madini, mafuta na gesi asilia ili kumpa mamlaka ya moja kwa moja

Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa hesabu za Serikali kupata taarifa zitakazosaidia ukaguzi wake kwa maslahi mapana ya nchi<sup>11</sup> <sup>12</sup>

Pia, Serikali ifanye upya mapitio ya sheria hizi kumuwezesha CAG kupata taarifa za makampuni ya madini na mafuta ukizingatia Ushahidi tosha ulioonyeshwa kutokana na kilichotokea kati ya TPDC na makampuni ya uwekezaji ya China

### C. UWEZESHAJI WAZAWA (LOCAL CONTENT)

Kwa kupitia Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na kanuni zake, kampuni za uchimbaji madini Tanzania zinapaswa kuandaa na kuwasilisha mpango wa uwezeshaji wazawa katika baraza la uwezeshaji wananchi kiuchumi. Pamoja na masuala mengine, mpango huo utapaswa kuonesha namna kampuni za wananchi (wazawa) zitapata vipaumbele katika zabuni na bidhaa zinazopatikana nchini, upatikanaji wa ajira kwa watanzania na utoaji wa mafunzo ya kuwajengea uwezo zaidi waajiriwa wazawa. Hatua hii ina nia njema na yakupongezwa kwa sababu ina lenga kuwashirikisha wananchi kuwa sehemu ya uchumi ya madini ya nchi yao.

Changamoto tunazoziona ni uwezo na umahiri/ushindani usioridhisha wa kampuni za wazawa kushiriki kikamilifu katika fursa hizo, na pia kukosekana kwa muunganiko (Link) wa mnyororo wa thamani baina ya kampuni za madini na sekta zingine za kiuchumi, kama kilimo, uvuvi, elimu na ufundi n.k, pia uelewa mdogo wa wananchi kuhusu uwepo wa fursa hizo.


Pendekezo letu ni kwa Serikali kuweka mifumo na mikakati inayoteklezeka kwa ajili ya kuwaandaa wananchi na kuwajengea uwezo ili washiriki kikamilifu katika sekta ya madini kwa kushirikiana na wadau na taasisi mbalimbali za maendeleo zikiwemo asasi za kiraia.

### D. UWAJIBIKAJI WA MAKAMPUNI KWA JAMII (Corporate Social Responsibility)

Katika suala la uwajibikaji wa makampuni kwa jamii, kifungu cha 102 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, (Kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Anuai Na. 7, 2017) kinafanua wajibu wa makampuni kujihusisha katika huduma za kijamii katika maeneo ambayo shughuli za uziduaji zinafanyika. Sheria pia inaelekeza kuwa, Kila mwaka kampuni hizi zinapaswa kuandaa Mpango wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (Plan for Corporate Social Responsibility), ambao utapelekwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa/ Vijiji/ Halmashauri kwa ajili ya majadiliano na kupitishwa ili uanze kutekelezwa katika eneo husika.

<sup>11</sup> CHANZO: Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu wa Serikali

<sup>12</sup> FROM TRANSPARENCY TO IMPROVED REVENUE COLLECTION AND MANAGEMENT IN THE EXTRACTIVE SECTOR IN TANZANIA (HakiRasilimali working Paper, 2019)




Ni jambo jema na lenye nia nzuri la kuwawezesha wananchi kupata huduma za kijamii zinazohitajika katika maeneo yao. Ingawa, changamoto kubwa zilizopo zinahusisha baadhi ya makampuni kutokutekeleza majukumu yao kama inavyotakiwa kisheria, pia, uwepo wa migongano ya uelewa kwa baadhi ya makampuni na halmashauri, ambapo, baadhi ya makampuni hudhani suala la mipango ya nini kifanyike ni suala lao pekee, ilhali, baadhi ya Halmashauri zikiamini kuwa wao ndio wanaopaswa kupanga na kipeleka mipango yao katika kampuni husika ili zitoe fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mipango yao. Halikadhalika, kutokuwepo kwa kikomo (asilimia) cha kiwango kinachotakiwa kutumika katika shughuli za uwajibikaji wa makampuni kwa jamii inapunja jamii za maeneo husika kufaidika na rasilimali zao.<sup>13</sup>

Hivyo basi, tunashauri na kupendekeza, kuandaliwa kwa kanuni/ Mwongozo wa ngazi ya Taifa utakaofafanua masuala kadhaa yakiwemo majukumu na wajibu wa wadau mbalimbali katika jamii yakiwemo makampuni na halmashauri husika.

<sup>13</sup> Mganda V (2016): Challenges on Corporate Social Responsibilities in the Mining sector in Tanzania; The case study of Bulyanhulu and Geita Gold Mining. Business Education Journal Volume 1 issue No. 2.

## E. UCHIMBAJI MDOGO

Uwezesaji wa wachimbaji wadogo ni moja kati ya maeneo muhimu na ya vipaumbele katika Sheria ya Madini ya mwaka 2010, (Kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Anuai Na. 7, 2017). Uchimbaji mdogo umetengeneza ajira kwa watu wengi na unaweza kunufaisha zaidi wananchi wengi na nchi kupata mapato yatokanayo na kodi na tozo mbalimbali katika rasilimali madini. Kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Madini, kati ya julai, 2018 hadi februari, 2019, leseni za uchimbaji mdogo 4,497 zilitolewa na Tume ya madini kwa wachimbaji wadogo.



Hatua ya Serikali kuitia Wizara ya madini ya kuanzisha utoaji wa ruzuku kwa wachimbaji wadogo na wakati na pia kufuta kodi ya ongezeko la thamani na kodi ya zuijio kwa wachimbaji wadogo, ni hatua za kupongezwa kwani zinalenga kuwawezesha wachimbaji wadogo. Hivyo basi, pamoja na jithada zinazochukuliwa na Serikali za kushughulikia kero zinazowakabili wachimbaji wadogo ili kuondokana na kutumia zana duni katika


uchimbaji, ukosefu wa masoko ya uhakika ya madini, maeneo madogo, migogoro, ukosefu wa mitaji, n.k. Itakuwa ni vyema kwa Serikali kuitia Wizara, Tume ya Madini na STAMICO, kuendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo kwa kuwakopesha zana za uchimbaji, kuwapatia utaalamu na matumizi ya teknolojia katika uchimbaji na uchenjuaji wa madini, pia, kuwapatia mafunzo ya ujuzi, huduma za utafiti, teknolojia, mitaji na hasa kuanzisha benki ya madini au kuwadhamini ili waweze kupata mikopo yenye masharti na riba zisizoumiza.

### MAPENDEKEZO YA JUMLA KUTOKANA NA UCHAMBUZI HUU

Kwa kuzingatia umuhimu wa Sekta ya madini, mafuta na gesi asilia nchini pia manufaa ambayo yanawenza kupatikana kwa ajili ya nchi na wananchi katika eneo hili tunapenda kutoa mapendekezo yetu katika maeneo ambayo tunaamini yatakuwa na manufaa makubwa katika vipaumbele vya bajeti ya mwaka 2019/2020, kama ifuatavyo:-

#### 1: MGAWANYO WA BAJETI YA TAIFA KWA UJUMLA:

Hofu yetu ni kwamba uelekezaji wa rasilimali nyingi kwenye miradi michache kunaweza kusababisha kudumaa kwa miradi mingine ya maendeleo utakaosababishwa na ufinyu wa mgawanyo wa rasilimali.



Kuwepo na utaratibu unaozingatia mgawanyo wa rasilimali wenyewe uwiano unaofaa ili kutoa fursa kwa sekta zingine kushamiri. Kwa mafano, Makadirio ya bajeti ya 2019/2020 katika sekta ya Nishati na ujenzi yanachukua zaidi ya asilimia 50 ya bajeti yote ya nchi, hii inaweza kufaya sekta zingine kutopata rasilimali fedha za kutosha kwa shughuli za maendeleo. Halikadhalika, pamoja na kutambua umuhimu wa sekta husika, tunashauri utekelezaji wa miradi hiyo kugawanywa katika vipindi vya muda ili kuruhusu mgawanyo wa wastani kuelekezwa katika miradi hiyo.

## 2: UTUNZAJI WA MAZINGIRA:

Tunashauri kuwa Wizara ya Nishati na Serikali kutekeleza mpango kabambe wa TPDC (NGUMP 2016) ili kuwezesha miundombinu ya gesi asilia kujengwa ili kuharakisha matumizi ya gesi asilia katika kaya na pia kupunguza mahitaji na matumizi ya Mkaa na Kuni hasa kwa mikoa mikubwa ambapo mahitaji huongezeka kila siku kwa ajili ya shughuli za kiuchumi.



Kwa kutambua kuwa kuna baadhi ya migodi inatarajia kufungwa, mathalani, Bulyanhulu, n. k. Tunaishauri Serikali kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya tathmini ya athari za kimazingira katika meneo ya miradi mikubwa na taarifa za athari hizo ziwekwe bayana ili kuelimisha wananchi hasa wanaoishi kando kando ya miradi hiyo kuchukua tahadhari za kiafya na maisha yao.

Vivyo hivyo taasisi zingine kama Asasi za Kiraia (AZAKI) na Taasisi za kitaaluma pia wafanye tafiti sambamba zenyelengo la kubaini athari za kimazingira ili kuchangia katika juhudzi za Serikali katika utunzaji wa Mazingira.

Kwa kuzingatia Mwenendo wa mabadiliko ya tabianchi (trends of climate change), na jitihada za Serikali kufufua na kuwekeza katika eneo la madini ya makaa ya Mawe, tunaishauri Serikali kuititia upya Sheria za usimamizi wa mazingira ili kuepusha madhara / athari hasi zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi.

### 3: MRADI WA KUSAMBAZA NA KUUZA GESI

Tunashauri kwamba kwa maeneo ambayo gesi ilishaanza kuvunwa ambako ni Mnazi Bay na Songosongo, Serikali iwe na mkakati kabambe wa kuuza gesi kwa ajili ya matumizi mbalimbali,

takwimu<sup>14</sup> zinaonesha kuwa gesi inayotumika kwa mwaka mzima ni kati ya asilimia 4.18 na 6 tu ya uwezo wa bomba. Hii ni hasara kwa taifa ikizingatiwa kuwa bomba la gesi limejengwa kwa mkopo na tayari mkopo na riba umeanza kulipwa.

Pia, Serikali itoe kipaumbele katika uwekezaji wa vitalu vya kimkakati vya gesi asilia vilivyopo chini ya mamlaka ya TPDC kwa kuharakisha mazungumzo na wawekezaji ili kufikia muafaka wa kupata uwekezaji wenye manufaa na pia kujali muda kwa kutumia fursa ipasavyo. Kuendelea kuchelewa kuwekeza kunaweza kutoa fursa kwa nchi zingine zenye gesi kama Msumbiji kukosesha taifa faida nono.

TPDC iweke juhudzi za kutosha katika utafutaji wa masoko ya uhakika kwa ajili ya usambazaji wa Gesi Asilia. Katika bajeti ya mwaka 2018/19 takribani viwanda 10 vilikuwa vimeunganishwa au vilikuwepo katika majadiliano. Pia kwa mwaka huo kulikuwa na Matarajio ya kuunganisha kaya/nyumba Zaidi ya 2000 katika miundombinu ya gesi asilia. Kwa vyovoyote vile, shabaha hizo bado haziridhishi ukizingatia wingi wa viwanda vilivyopo Nchini na idadi ya kaya zilizopo. Tunashauri Serikali iwekeze na kuiwezesha TPDC kufikia malengo zaidi.

#### **4: MPANGO WA TAIFA WA UWAJIBIKAJI WA MAKAMPUNI NA UWEZESHAJI WAZAWA**

Ili nchi iweze kunufaika na rasilimali zake, tunaishauri Serikali kundaa mpango kabambe utakao toa mwongozo kuhusu uwajibikaji wa makampuni kwa jamii na Uwezeshwaji wazawa. Tunaamini kuwa kama Mpango huu utafikiwa, utaweza kutoa viwango elekezeki vitakavyoweza kuunganisha sekta zote na faida jumuishi kwa Taifa.

#### **5: MUUNDO WA WIZARA YA MADINI**


Kuna haja ya kupitia upya muundo wa Wizara ya Madini na kufanya marekebisho katika idara au taasisi ambazo zinaonekana kuwa na majukumu yanayofanana. Kwa minajili hii, kuanzishwa kwa Tume ya Madini kwa mujibu wa marekebisho ya Sheria ya Madini 2010, inapokonya mamlaka na kazi ambazo idara ya madini chini ya kamishna wa madini alikuwa nazo. Kuendelea kuwa na idara na taasisi ambazo zinafanya kazi zinazofanana siyo tu kwamba zinatoa taarifa ya utendaji unaofanana ila pia ni kuingia għarama zisizo na tija.

#### **6; MATAMKO YA KISIASA NA UTEKELEZAJI WA BAJETI**

Kwa kuzingatia utawala wa Sheria, taratibu na kanuni za nchi, matumizi yote ya Bajeti ya Serikali yanapaswa kupitishwa na Bunge kwa niaba ya Wananchi<sup>15</sup>. Kupitia vyombo mbali mbali vya Habari, mawasilisho Bungeni, kumekuwa na matamko mbalimbali ya kisiasa yenye athari kwenye Utekelezaji wa Bajeti kama zinavyopitishwa na Bunge. Kwa mantinki hiyo ni kwamba Bajeti elekezi zimekuwa hazifikii lengo husika. Ili kuwepo na bajeti inayozingatia ukomo na uhalisia endeleuvu, tunashauri kuwa matamko ya kisiasa yanayoongeza għarama na bajeti ambazo hazikuwepo awali kudhibitiwa ili rasilimali fedha zitumike kwa vipaumbele vinayotakiwa na siyo vinginevvo.

<sup>14</sup> CHANZO: Taarifa Mdhibit na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ya mwaka (2017/18)-Mashirika ya Umma

<sup>15</sup> CHANZO: Katiba Ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 136 (1a & b))



Hivyo basi wanasiassa, watendaji wa Serikali hawana budi kuzingatia Sheria, taratibu na kanuni za nchi katika usimamizi na Utekelezaji wa Bajeti.

Ukinzani wa uhalisia wa Bajeti na matamko ya kisiasa siyo tu husababisha hasara, lakini pia huondoa imani ya wananchi kwa viongozi wao na Serikali kwa Ujumla.<sup>16</sup>

#### Tamko Hili limeandaliwa na kutolewa na HakiRasilimali

Kwa maelezo Zaidi, wasiliana nasi kuititia

[info@hakirasilimali.or.tz](mailto:info@hakirasilimali.or.tz)

Simu: +255 (0) 745 655 6555

[www.hakirasilimali.or.tz](http://www.hakirasilimali.or.tz)

<sup>16</sup> CHANZO: Katiba ya Jamuhuri Ya Muungano wa Tanzania (1977 ) Ibara ya 8 (a)(b)(c)

### ANNEX 1: MATRIX OF ISSUES TO FURTHER SCRUTINY, RESEARCH AND ANALYSIS (Working document)

Issue	CHANGAMOTO / CHALLENGE	Solution
<b>Ufinyu wa Bajeti</b>	1) Fedha za maendeleo hazitoki au zikitoka zinakua kidogo sana na zinachelewa kutoka.	1) Kubadilisha vipaumbele 2) Kuboresha ukusanyaji wa mapato mfano, Wizara ya Nishati haionyeshi taarifa ya ukusanyaji wa maduhuli kwa 2018/19.
<b>Ukosefu wa fedha za maendeleo</b>	Mfano: Hadi kufikia februari, 2019, inaonekana hakukua na fedha yoyote iliyotolewa kwa ajili ya maendeleo kwenda TEITI. Ukosefu huu wa fedha unaleta changamoto katika kukuza uwazi na uwajibikaji.	1: Serikali waweke kipaumbele kuitengea TEITI Fedha za kutosha ili kukuza uwazi na uwajibikaji kwenye sekta ya madini mafuta na gesi.
<b>TEITI (Mpango wa kukuza Uwazi na Uwajibikaji Nchini)</b>	5) Taarifa kuu ya TEITI ya utekelezaji kwa mwaka 2016/17 na 2017/18 hazijatolewa hadi leo, ingawa, kuna maelezo ya kuanza kwa utaratibu wa kumtafuta mtaalamu mshauri wa kuandaa taarifa husika. Ingekuwa vyema kwa TEITI kutoa mrejesho wa hatua zilizofanyika katika kutekeleza jukumu la utolewaji wa taarifa tajwa.	1) Serikali ifanye marekebisho ya Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika rasilimali za madini, mafuta na gesi asilia ya Mwaka 2015 ili kuiwezesha TEITI kuwa Taasisi iliyo huru na yenye muundo na mfumo mpana unaoiwezesha kuwa na mamlaka katika kukusanya rasilimali fedha na kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati.
<b>1) Taarifa ya 9 na 10 ya TEITI</b> <b>2) Rejista ya Wamiliki halali (Beneficial Ownership) sio shareholders kama serikali inavyowaita</b>	6) Kuanzishwa kwa rejista ya taarifa kwa Umma kuhusu wamiliki halali katika kampuni za madini, mafuta na gesi asilia ni moja kati ya shughuli iliyopaswa kutekelezwa, ila hakuna maelezo yoyote katika taarifa kuhusu hatua za utekelezaji wa uanzishwaji wa rejista hiyo kama ilivyositisizwa na aliyekuwa Waziri wa Madini, Mh. Angella Kairuki tarehe 25/10/2018, jijini Dodoma wakati akizindua	2) Kupitia Maagizo ya Mh. Wazir wa Mkuu na aliekua Wazir wa

<p><b>3) Uwazi kwenye matumizi ya mapato ya Halmashauri</b></p> <p><b>4) Mratibu wa TEITI kutoajiriwa hadi leo</b></p> <p><b>5) SPECIAL AUDIT kuhusu discrepancy ya shilling 30.5 billion iliyogunduliwa kwenye report ya 8 ya TEITI</b></p>	<p>kamati ya tatu ya TEITI. Rejista ina umuhimu mkubwa katika kuboresha uwazi katika sekta hii na pia itasaidia kuzuia upotevu wa rasilimali na mapato yatokanayo na rasilimali madini, mafuta na gesi asilia. TEITI haina budi kutoa mrejesho kwa Umma kuhusu hatua iliiyofikiwa ya uanzishwaji wa rejista.</p> <p><b>7) Taarifa ya TEITI imeonesha mionganoni mwa mafanikio kwa mwaka 2018/19 ilikuwa ni kuongezeka kwa uwazi wa matumizi ya mapato ya halmashauri yanayotokana na TOZO kutoka kampuni za uchimbaji madini, mafuta na gesi asilia. Ingawa hakuna maelezo ya kutosha kuonesha ni halmashauri zipi na iwapo ongezeko hilo ni kwa kiasi gani ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita.</b></p> <p><b>8) Ni Zaidi ya mwaka sasa toka watu wafanyiwe usaili kwenye nafasi ya MRATIBU WA TEITI cha kushangaza hadi leo hii, Mratibu huyo hayaajiriwa.</b></p> <p><b>9) Inavyofahamika ni kwamba CAG tayari alishaanza kuchambua report inayohusu SH. 30.5 Bilioni iliyojitokeza kwenye report ya 8 ya teiti, Changamoto kubwa inayomkibili ni kwa baadhi ya makampuni kama North Mara kutowashilisha taarifa zao kwa CAG. Na tunatambua report hiyo ya special audit inatakiwa iwe imeshafika bungeni kabla ya waziri hajasoma bajeti ya wizara yake.</b></p>	<p>Madini Angella Kairuki, serikali itoe taarifa ya maendeleo ya mchakato wa kuanzishwa kwa Rejista.</p> <p><b>3) Serikali kupitia wizara kutoa taarifa zenyne maelezo ya kutosha ili kusaidia watumiaji wa taarifa kuelewa kwa kina ni Halmashauri gani ambazo zinatajwa hapo juu ili iwe funzo kwenye halmashauri zingine ambazo hazifikia lengo.</b></p> <p><b>4) Serikali itoe taarifa ni lini Mchakato wa kuamuajiri mratatibu wa TEITI utakamilika.</b></p> <p><b>5) Serikali kupitia Wizara na TEITI ichukue hatua kuhakikisha taarifa zinazohitajika na CAG zinafika kwa wakati. Na ni kwa Nini North Mara hadi leo hawajapeleka taarifa zao?</b></p>
<p><b>Taarifa ya CAG juu ya baki ya fedha iliyotolewa na World Bank kwa ajili kutolewa ruzuku kwa</b></p>	<p>Hakuna taarifa kutoka wizarani juu ya fedha hizo. Hili linaibua maswali mengi kama fedha ziliwafikia wachimbaji wadogo, na fedha hizo zilikuwa ni kiasi gani. Lakini pia swali lingine ni kuwa kama zilitolewa ni wachimbaji gani walipata.</p>	<p>Wizara itoe taarifa sahihi na kwa wakati juu ya fedha hizo.</p>

wachimbaji wadogo wadogo.		
<b>TUME YA MADINI</b>		
<b>Makusanyo ya maduhuli</b>	<p>1: Wizara ya Madini kureport kukusanya maduhuri sawasawa na makusanyo yanayoripotiwa kukusanywa na Tume. Swali ni je ni kipi kimekusanywa na Wizara ya Madini au Tume ya Madini.</p> <p>2: Vivyo hivyo wizara ya Nishati kwenye report zao haionyeshi kiasi cha maduhuli kilichokusanywa kwa mwaka wa fedha 2018/19 lakini bado inaomba fedha kwa ongezeko la aslimia 55%.</p>	Wizara ya Nishati itoe taarifa xa utekelezaji wa Bajeti na makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2018/19.
<b>Muundo wa idara na taasisi nyingine</b>	<ol style="list-style-type: none"> <li>1. Tume haifahamiki vizuri kwa wadau na kupelekea kuleta mkanganyiko hasa kwa wachimbaji wadogo.</li> <li>2. Kuna uwezekano kukawa na mgongano wa kimamlaka kati ya Tume ya madini na Idara ya Madini iliyo chini ya wizara.</li> <li>3. Kumekuwa na uelewa tofauti ndani ya wizara juu ya majukumu ya Tume ya Madini na Idara ya madini</li> </ol>	<ol style="list-style-type: none"> <li>1) Majukumu na wajibu wa Tume ya Madini na Idara ya Madini yaainishwe washi</li> <li>2) Kuna haja ya kuwa na mabadiliko ya Sheria na muundo wa ndani juu ya majukumu ya Tume ya Madini na Idara ya Madini</li> </ol>

STAMICO	<p>STAMICO ni shirika la madini la Taifa ambalo linamilikiwa na serikali kuitia Msajili wa Hazina kwa hisa za asilimia 100%. Wakati huo huo STAMICO ina kampuni tanzu ya STAMIGOLD ambapo STAMICO inamiliki hisa kwa asilimia 99% na Serikali kuitia kwa Msajiri wa Hazina inamiliki hisa kwa asilimia 1%.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>1) Kwa mujibu wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali yam waka 2017/18 STAMIGOLD imekuwa ikijiendesa kwa hasara na kushuhudia uzalishaji wa dhahabu kushuka kwa 58% kwa kipindi cha mwaka 2015 -2018</li> <li>2) Mgodi wa STAMIGOLD umekosa huduma ya umeme wa TANESCO kwa muda wa miezi kadhaa na kupelekea kutumia umeme wa jeneretor ambao unaigharimu kiasi cha shilingi million 900 mpaka billion 1 kwa mwezi kuendesha shughuli zake. Hali Hii inachangia STAMIGOLD kuendelea kufanya uzalishaji usio na faida.</li> <li>3) STAMICO ilipewa kandarasi ya kokoto kwenye mradi wa SGR baada ya wabunge kupendekeza hivyo ili kuachana na mpango uliokuwa unatumika ambapo kokoto ziliwuwa zinaingizwa nchini kutoka Uturuki. Hata hivyo STAMICO ilikosa fedha ya kufanya kazi hiyo, kiasi ambacho kinakadiriwa kuwa dola za kimarekani 400,000.</li> </ul>	<p>1) Serikali kuitia Msajili wa Hazina iangalie uwezekano wa kuwa na mpango wa kufanya uwekezaji wa mtaji kwa STAMICO iliiweze kujiendesa kwa faida na kuweza kuziinua kampuni Tanzu zak.</p>
STAMICO NA HALI YA WAFANYAKAZI	<p>STAMICO na makampuni yake tanzu yamekuwa yanategeme a ruzuku toka seriaklini kwa ajili ya kujiendesa. Hali hii imapelekea makampuni hayo kujiendesa kwa hasara kubwa</p>	<p>Serikali iachane na mpango wa kuboresha STAMICO na badala yake Serikali ilenge kuboresha makampuni</p>

	<p>na kupelekea wabunge kushauri STAMICO kuvunjwa au isiruhusiwe kusimamia makampuni yake tanzu ili kuokoa hasara kwa Taifa.</p> <p>Mfano mdogo ni STAMIGOLD BIHARAMULO MINING LTD. Hii ni Kampuni inayomilikiwa na STAMICO. Hadi Mwezi February 2019 ilikuwa imeajiri wafanyakazi 350 na wengine wapatao 230 walikuwa wameajiriwa na kampuni ya kandarasi iitwayo JUNIOR CONSTRUCTION. Kutokana na mwenendo mbaya wa uzalishaji mgodini, wahanga wakubwa wa matatizo ya uzalishaji ni wafanyakazi. Wafanyakazi wanalamika kulishwa chakula cha aina moja yaani wali na maharage kila siku. Mishahara haitoki kwa wakati, wanapewa mikataba ya mwezi mmoja hadi miezi mitatu ambapo ni kinyume cha sheria ya Ajira na Mahusiano kazini Na.6/2004.</p> <p>Kutokana na kusuasua kwa ulipaji wa mishahara, pia michango ya pensheni haipelekwi kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Hadi kufikia Mwezi February 2019, licha ya wafanyakazi kukatwa 10% kwa ajili ya kuchangia mifuko ya hifadhi ya jamii, Mwajiri alikuwa amelimbikiza michango ya miezi 22. Wafanyakazi walioachishwa kazi wanapata shida sana wanapokwenda kufuatilia mafao yao kwani huambiwa kuwa mwajiri wao hajapeleka michango hivyo hawawezi kufungua madai.</p> <p>Mapema mwezi Machi, wafanyakazi sita hawakuongezewa mkataba, walipouliza michango yao wakaambiwa haijaenda</p>	<p>tanzu ya STAMICO ili makampuni hayo yenyewe yaweze kuwa na uwezo wa kuijidesha badala ya kutegemea ruzuku kutoka serikali.</p>
--	---	---

	kwa miaka miwili na nusu, wakakataa kuondoka mgodini, waliondolewa na polisi na kuwekwa ndani siku mbili na baadae walitolewa kwa dhamana. Hali ni mbaya sana.	
<b>Sera ya Mahusiano ya Kimataifa iliyojikita katika diplomasia ya kiuchumi</b>	Sera ya mahusiano ya nje ya Tanzania imejikita katika diplomasia ya kiuchumi. Hali ya uwekezaji katika sekta ya uziduaji ambayo ndio inaleta uwekezaji wa moja kwa moja wan je (FDI) haiakisi sera hii ya mahusiano ya nje. Kuna haja ya kujua ni FDI ngapi zimefanyika na ngapi zimesimamisha uwekezaji wao katika kipindi cha mwaka 2015-2019 kutokana na mabadiliko ya sharia zetu yaliyofanywa mwaka 2017. Mfano mzuri ni sharia ilivyoweka ni kwa namna gani wawekezaji wanaweza kufikia usuluhishi wa taasisi za kimataifa za usuluhishi.	Serikali ipitie upya sheria hasa kipengele kinachomkataza mwekezaji kufikia taasisi za kimataifa za usuluhishi.
<b>Majadiliano yasioisha kwenye miradi ya gesi na mafuta</b>	Kwa taarifa tulizonazo, kampuni ya Equinor hadi sasa imegundua gesi yenyeye ujazo wa takribani 20TCF. Wamekuwa tayari kujenga LNGP tangu mwaka 2014, lakini majadiliano baina yake na serikali hayajafika mwisho. Katika harakati za kujihakikishia usalama wa kibashara, pamoja na mambo mengine, tumeshuhudia wakibadili jina kutoka STATOIL na kuwa EQUINOR, haya hayawezhi kuwa mabadiliko ya bahati mbaya bali ya kimkakati. Lakini tumeshuhudia pia kwamba, mwaka huo huo, kampuni hii imefanya “bid” kupewa mradi wa umeme wa nguvu za Jua huko Singida. Kutokana na uzoefu wao katika masuala haya ya nishati kuna uwezekano mkubwa sana wa kupata tenda ya kujenga mradi wa nguvu za juu. Hii	1) Serikali iweke wazi sababu za ucheleweshaji wa utekelezaji wa mradi wa gesi

	inaweza kupelekea Equinor kujikita zaidi kwenye uwekezaji wa umeme wa nguvu za juu na kuachana na mradi wa gesi.	
<b>Vipaumbele vya Taifa</b>	<ol style="list-style-type: none"> <li>1. Kuna haja ya kufahamu kama Wizara ya Nishati ina mkakati ulio wazi wa utekelezaji wa miradi mbalimbali kulingana na vipaumbele vya kitaifa.</li> <li>2. Kuna utekelezaji wa miradi mikubwa ya nishati unaofanyika kwa sasa nchini, ikiwa ni miradi ya gesi pamoja na mradi wa bonde la mto Rufiji. Je wizara ya Nishati ina uwezo kiasi gani wa kusimamia miradi hii mikubwa?</li> <li>3. Serikali inatumia fedha za kibiashara (commercial funds) kutoka mabenki ya ndani kama CRDB kutekelenza miradi yake kama Mradi wa Bonde la Mto Rufiji.</li> </ol>	<ol style="list-style-type: none"> <li>1) Wizara ya Nishati iandae Mapango Mkakati wa utekelezaji wa miradi ya nishati</li> <li>2) Wizara ya Nishati ianishe bayana vipaumbele vya taifa katika utekelezaji wa miradi ya nishati nchini</li> </ol>

<b>EACOP</b>	<ol style="list-style-type: none"> <li>1. Nani anaproduce umeme kuipatia TANESCO kwa ajili ya kusambaza ya umeme kwenye bomba la Mafuta?</li> <li>2. Serikali pia inaomba ongezeko la profit kutoka bomba la mafuta kuzidi hata profit wanayotakiwa Kupata wazalishaji mafuta yanakotokea?</li> <li>3. Hadi leo Host Government Agreement inasuasua</li> <li>4. Uzoefu wa compensation kwenye migodi ya madini imekua ni Changamoto, je itakuaje tofauti kwenye Miradi ya bomba?</li> </ol>	
--------------	---	--

<p><b>Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kutokuwa na nguvu za kukagua hesabu za makampuni ya uziduaji</b></p>	<p>1. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ana nafasi ndogo sana ya kufanya ukaguzi kwenye makampuni ya uziduaji, kinyume cha Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na kifungu cha 5 na 15 cha Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma yam waka 2008, juu ya upatikanaji wa taarifa na watu. Vifungu hivi vya sheria vinaingiliwa na kifungu cha 26 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na mabadiliko yake yam waka, na kifungu cha 93 cha Sheria ya Mafuta ya mwaka 2017, vifungu ambavyo vinakataza taarifa a makampuni ya madini na mafuta kutolewa kwa mtu wa tatu isipokuwa tu kwa ridhaa ya wamiliki wa mgodi au wa leseni au haki ya uchimbaji. Ibara ya 18 (k) ya makubaliano ya mfano ya kubadilishana taarifa za utekelezaji (the model production sharing agreement of 2013 (MPSA 2013) yanaruhusu serikali kupitia kwa wawakilishi wake waliopewa nguvu kupata taarifa za mikataba. Ofisi ya CAG iliomba taarifa kutoka Wizara ya Nishati na Kampuni ya Taifa ya Mafuta (TPDC) na kuchukua takribani miezi miwili, mnamo mwisho wa mwezi Februari na kuchangia kushindwa kwa CAG kufanya ukaguzi wa rekodi za kampuni kwenye allowable and receivable costs na mapato yaliyopatikana ili kuweka kwenye ripoti yam waka 2016/17.</p>	<p>Serikali ifanye upya mapitio ya sheria hizi kumuwezesha CAG kupata taarifa za makampuni ya madini na mafuta ukizingatia Ushahidi tosha ulioonyeshwa kutokana na kilichotokea kati ya TPDC na makampuni ya uwekezaji ya China.</p>
---	---	--

	2. Kwa nini sheria hizi mbili zinamuona CAG kama mtu wa tatu (third party) wakati ofisi ya CAG ni ofisi ya umma. Lengo/nia hasa ya sheria hizi ilikuwa nini kufanya hivyo?	
<b>Uwezesaji wazawa (Local Content)</b>	Kuna haja ya kuwa na Sera ya Taifa ya Uwezesaji Wazawa ili kutoa mwongozo wa kufuatwa na kuwa sera mtambuka kwa sekta zote katika mnyororo wa thamani.	Serikali itunge Sera ya Taifa ya Uwezesaji wa Wazawa.
<b>Uwajibikaji wa makampuni kwa jamii (corporate social responsibility)</b>	<p>a. Kukosekana kwa ushirikishwaji wa wawakikishi wa wananchi katika kupanga mipango ya maendeleo yanayotegea michango hii ya CSR. Wakuu wa Mikoa wanaonekana kufanya maamuzi badala ya vikao rasmi vilivyowekwa kisheria.</p> <p>b. Jambo la pili ni mnning'inio (hangover) ya utaratibu wa zamani, ambapo makampuni yalizoea kufanya kazi na host communities moja kwa moja. Kwasababu maamuzi mengi yanapofanyika hayawashirikishi wanufaika (wananchi) wanajikuta wakilalamika wakiamini kuwa kampuni inawadhulumu.</p>	Maamuzi ya matumizi ya pesa hizi yaamuliwe na vikao rasmi bila kuingiliwa na wanasiasa. Lakini pia elimu juu ya mabadiliko ya sheria na uratibu wa CSR Itolewe kwa wanufaika.
<b>Mazingira</b>	Kwa mujibu wa taarifa mgodi wa Buzwagi unakaribia kufungwa. Je kuna fedha kiasi gani zilizotengwa kama rehabilitation fund kwa ajili ya kurudisha mazingira katika hali yake ya awali na lini fedha hizo zitatumwa katika halmashauri husika. Hili pia linakwenda kwa mgodi wa Bulyanhulu ambao umefungwa kwa muda wakati majadiliano yakiwa yanaendelea.	Taarifa za fedha za rehabilitation fund kwa mgodi wa Buzwagi na Bulyanhulu ziwekwe bayana kuzisaidia halmashauri husika zianze kutengeneza mikakati ya utekelezaji wake.
<b>Mwenendo wa kisheria kwenye sector</b>	(i) Article 22 (a) of the MPSA 2013 requires ownership of all fixed assets that were owned by the Contractor	The government to use Section 4 of the Natural Wealth and Resources

	<p>in petroleum operations to be transferred to the government (TPDC) at the expiration or termination of the agreement or when full costs of acquiring the assets have been recovered by the Contractor out of cost oil/gas. This also applies when more than 50% of the cost of a physical asset has been recovered and where TPDC has paid unrecovered portion of the asset. In this case, TPDC can elect to have the asset title transferred. The CAG report noted that MDAs do not provide for transfer of the mining assets. For example, Harvest Tanzania Ltd, on 3<sup>rd</sup> March 2018 issued a notice to conduct public auction to liquidate Acacia mining assets, inventory and plant at Buzwagi and in November 2013, STAMICO acquired Tulawaka Gold Mine and exploration licenses from Barrick Gold at a price of USD 4.5 million. These two deals were contrary to the MPSA 2013.</p>	<p>Contracts (Review and Renegotiation of Unconscionable Terms) Act of 2017 to amend all MDAs to implement the MPSA 2013 requirements, and to form special task committee to investigate all transactions that contradict the MPSA 2013.</p>
<p>TPDC na</p> <ol style="list-style-type: none"> <li><b>Utoaji wa fedha za maendeleo na leseni za kutafuta mafuta</b></li> <li><b>Acquiring of the 3D seismic data for deep sea blocks 4/1B and 4/1C</b></li> </ol>	<ol style="list-style-type: none"> <li>Katika sekta ya mafuta na gesi asilia kitalu cha 4/1B na 4/1C vitengwa kwa ajili TPDC mnamo mwezi Mei 2016, ambapo ilipeleka mapendekizo ya mpango kazi na makadirio ya chini ya utafutaji mafuta kwa kipindi cha miaka 4, kwa kiasi cha chini cha dola za kimarekani milioni 50 kwa kila kitalu kwa kila kipindi cha miaka miwili (na kufanya jumla ya dola za kimarekani milioni 200). Kwa mujibu wa CAG hakuna leseni ya utafutaji</li> </ol>	<p>TPDC na Wizara kuandaa na kutia saini makubaliano ya hiyari (MOU) ambayo yataongoza shuhjuli za utafutaji mafuta, utoaji wa wakati wa leseni za utafutaji mafuta na kuweka mikakati ya upatikanajifedha kwa ajili ya mradi.</p>

	<p>mafuta imetolewa kwa TPDC kwa ajili ya kufanya shughuli hiyo. Lakini pia HAKUNA pesa zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji. Hii inachlewesha Serikali kupata faida ya upatikanaji wa mafuta na kuvutia wawekezaji.</p> <p>2. TPDC haijapata data za ki-seismic za 3D kwa ajili ya kina kirefu baharini kwa vitalu 4/1B na 4/1C ili kuwavutia wadau kwa ajili ya utafutaji mafuta, kwa sababu ya mabadiliko ya kiteknolojia ambayo yanataka kuborehsa seismic data za 2D. katika fedha kiasi cha shilingi bilioni 4.5 zilizotengwa kwa ajili ya zoezi hilo, ni shilingi milioni 24.8 tu ndizo zilizotolewa na serikali (sawa na aslimia 0.6%). Kupata data za ki seismic za 3D ni muhimu kwa ajili ya kuwezesha utafutaji mafuta na kuvutia wadau wa utafutaji mafuta.</p>	
<b>Mchakato wa tenda kwa sekta ya uziduaji na upotevu wa shilingi mikioni 443</b>	<p>Mchakato wa tenda wa mwezi Oktoba mwaka 2013 kwa ajili ya utafutaji mafuta na gesi kwenye kina kirefu na vitalu vya extraction na kimoja cha Kaskazini mwa Ziwa Tanganyika, wakati wa mzunguko wa nne wa utoaji wa leseni za mwambao, na kwa mujibu wa makubaliano ya mfano ya kubadilishana taarifa za utekelezaji ya mwaka 2013 (MPSA 2013) ulihusisha zabuni kutoka kwa makampuni mawili ya China National Offshore Oil Corporation na Ras Al Khaimah Gas LLC, ambazzo haz ikufanikiwa. CAG aliona kwamba wawekezaji hawakuwa wanaamini masharti ya MPSA ya mwaka 2013, ambapo</p>	TPDC iishauri Serikali kupitia upya masharti yaliyo chini ya MPSA ya mwaka 2013 na kutoa upya tangazo la zabuni.

	Serikali ilipoteza shilingi milioni 443 kwa mchakato wa zabuni ambao haukufanikiwa. Zaidi ya hayo, hakuna tangazo lingine la zabuni.	
<b>Hisa za TPDC</b>	Kifungu cha 44(5) cha Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015 inaitaka TPDC kushikilia kwa kiasi cha chini hisa za ushiriki kwa asilimia 25 ya haki zilizotolewa za mafuta. Hata hivyo, TPDC inashikilia ASILIMIA 20% tu chini ya Mnazi Bay na ASILIMIA 0% chini ya Songosongo na viwanja vya gesi vya Kiliwani Kaskazini.	Serikali itumie Kifungu cha 4(1) cha Sheria ya Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Renegotiation of Unconscionable Terms) Act 2017 kuchukua na kushikilia kiasi cha chini cha hisa za ushiriki kwa leseni zote za maendeleo.
<b>Mkopo wa huduma (Service Loan) uliotolewa na EXIM BANK na TPDC</b>	TPDC na TANESCO ziliingia kwenye makubaliano ya mauzo ya gesi (GSA) mnamo mwezi Septemba mwaka 2015 ambapo TANESCO ingekuwa inanunua gesi asilia kutoka TPDC kwa ajili ya uzalishaji wa umeme (kwa mitambo ya umeme ya Kinyerezi, Ubungo II and Symbion). Kwa kiasi chote cha invoice cha kiasi cha shilingi billion 567.5 (kati ya Septemba 2015 na Desemba 2017), TANESCO ililipa kiasi cha shilingi bilioni 318.9 tu (asilimia 56%), na kubakiza shilingi bilioni 248.6 hazijalipwa, na kudhoofisha uwezo wa TPDC wa kulipa mkopo uliotolewa na EXIM Banka ya China kutengeneza bomba la gesi la Mtwara-Dar es Salaam, na kuhatarisha kuhamishia haki za TPDC chini ya GSA kwenda EXIM Bank ya China.	